**Imehuishwa mara ya Mwisho tarehe: 31 Desemba 2025**

Masharti haya ya Jukwaa la Huduma ya Usafiri Mtandaoni yanawahusu watu binafsi na taasisi ("Watoa Huduma") wanaojisajili na Jukwaa la Bolt kupata na kuhakiki fursa zilizopo Tanzania kutoa Huduma ya Usafiri Mtandaoni kwa Wateja kwa niaba yao wenyewe.
Maneno na misemo yaliyoandikwa kwa herufi kubwa katikaMasharti haya ya Jukwaa yana maana kama ilivyotolewa kwenye farahasa kwenye kipengele cha 17 hapa chini.

Unaweza kupakua toleo la nje ya mtandao la Masharti haya ya Jukwaa kwa ajili ya kumbukumbu na matumizi yako ya baadae hapa

Muhimu: Kama wewe ni dereva unayetembelea Jukwaa la Bolt kupitia na kutoa Huduma ya Usafiri Mtandaoni kwa niaba ya mtu mwingine au taasisi, basi:
◦ huyo mtu mwingine au taasisi atakuwa Mtoa Huduma kwa malengo ya Masharti haya ya Jukwaa; na
◦ uhusika wako utakuwa na Mtoa Huduma, kama Dereva Aliyeteuliwa, kwa masharti yaliyokubaliwa baina yenu.

**1. Kuhusu Bolt na uhusiano na wewe**
1.1. Bolt inaendesha Jukwaa mtandaoni ndani ya Tanzania ('Jukwaa la Bolt') unaounganisha na kulinganisha watoa huduma za usafiri wanaojitegemea ("Watoa Huduma") pamoja na wateja watarajiwa ('Wateja')
1.2. Kama Mtoa Huduma, unaweza:
1.2.1. (kama ni mtu binafsi) kujisajili kama Dereva kupata na kuhakiki fursa za kutoa Huduma ya Usafiri Mtandaoni kwa niaba yako; na/au
1.2.2. kusajili Madereva Walioteuliwa kupata na kupitia fursa kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni itakayotolewa kwa niaba yako, kulingana na kipendegele cha {6}
1.3. Unapaswa kulipa mrabaha kwa Bolt kutoka katika malipo utakayolipwa na Wateja waliounganishwa na Huduma za Usafiri Mtandaoni, kama ilivyotolewa katika kipengele cha {8}
1.4. Jukwaa la Bolt linakuwepo kwa matumizi yako kwa uamuzi wako. Masharti haya ya Jukwaahayamlazimishi mtu yeyote:
1.4.1. kufikia Jukwaa la Bolt kupitia fursa za kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni; au
1.4.2. kutoa au kutimiza Huduma yoyote ya Usafiri Mtandaoni.
1.5. Hakuna chochote katika Masharti haya ya Jukwaa kinachomzuia mtu yeyote kutoa huduma za usafiri nje ya Jukwaa la Bolt.
1.6. kwa kufikia Jukwaa la Blot, unakubali kuichagua Bolt kama wakala wako kwa lengo la kufanikisha mauzo ya Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa Wateja, kulingana na kipengele cha {7}
1.7. Tutachakata taarifa zako binafsi na taarifa binafsi za Madereva Walioteuliwa kulingana na notisi za usiri kwa Tanzania zinazopatika https://bolt.eu/privacy.

**2. Kuhusu Masharti haya ya Jukwaa na Jukwaa la Bolt**
2.1. Masharti haya ya Jukwaa:
2.1.1. yataanza kutumika na kukubana kuanzia tarehe 31.12.2025, au kutoka tarehe uliyojisajili kama Mtoa Huduma kwa mara ya kwanza – yeyote ya baadaye;
2.1.2. yataendelea kufanya kazi hadi yatakapositishwa na wewe au Bolt kulingana na kipengele cha {13}; na
2.1.3. yatachukua nafasi ya toleo lolote lililopita la Masharti ya Jukwaa, vyovyote vile

ilivyoelezwa.
2.2. Bolt inaweza kufanya mabadiliko kwenye Masharti haya ya Jukwaa/au Jukwaa la Bolt kwa kukupatia notisi ya angalau siku kumi na tano (15) kabla ya mabadiliko hayo hayajaanza kufanya kazi. Kama hautaafiki mabadiliko hayo, unaweza kusitisha uhusika wako na Bolt kulingana na kipengele cha {13}.
2.3. Bolt inaweza pia kufanya mabadiliko kwenye Masharti ya Jukwaa au matumizi yako ya Jukwaa la Bolt mara moja na bila kukupa notisi ya awali pale:
2.3.1. unakubaliana na mabadiliko;
2.3.2. tumefanya mabadiliko, maboresho au marejeo ya Jukwaa la Bolt ambayo ni kwa nia njema, kuboresha utendaji, au kwa ulinganisho hayana madhara makubwa kwa matumizi ya Jukwaa la Bolt;
2.3.3. tumefanya mabadiliko tofauti na yaliyotajwa kwenye kipengele cha {2.3.2}, kuanzisha muonekano wa muda mfupi kwa ajili ya kupima, kujaribu, kufikika kwa uharaka, kuhakiki au maendeleo;
2.3.4. mabadiliko yanahitajika kwa haraka ili kukidhi matakwa ya sheria au kanuni zilizopo; au
2.3.5. tumechukua hatua za haraka kwa ajili ya kukabiliana na hatari zinazoweza kutokea kwa Watumiaji, hatari za usalama wa mtandaoni (ikiwemo programu hasidi, barua taka au ukiukaji wa data ), au kazi haramu au kitendo cha uvunjifu wa sheria.
2.4. Pale ambapo Bolt atafanya mabadiliko kulingana na vipengele kuanzia {2.3.3} hadi {2.3.5} (kwa pamoja), itakutaarifu kuhusu mabadiliko haraka iwezekanavyo.
2.5. Maudhui na utendaji kazi wa Jukwaa la Bolt huwa vinatolewa katika msingi wa “kama ilivyo” na “kama inavyopatikana”. Kwa kufikia na kuruhusu wengine kufikia Jukwaa la Bolt, unathibitisha kuwa:
2.5.1. Bolt haikuhakikishii, waziwazi au kwa kudokeza, juu ya uwepo wa Jukwaa la Bolt, maudhui yake au utendaji kazi wake; na
2.5.2. Bolt inaweza mara kwa mara kubadili muonekano uliopo kwa muda mfupi katika hatua ya kujaribu, kujaribu, kufikika kwa haraka, kuhakiki au maendeleo.

**3. Haki zako kufikia Jukwaa la Bolt**
3.1. Chini ya Masharti haya ya Jukwaa, tunakupa haki ya kutumia Jukwaa la Bolt isiyo ya kipekee, bila kizuizi, inayoweza kubatilishwa, na bila mrabaha, kwa madhumuni ya:
3.1.1. kufikia na kupitia fursa ili kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni; na
3.1.2. kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa kadri ya hiyari yako.
3.2. Haki iliyotolewa chini ya kipengele cha {3.1} inajumuisha uwezo wa kuwapatia Madereva Wateule haki ya kutumia Jukwaa la Bolt isiyo ya kipekee, bila kizuizi, inayoweza kubalitilishwa na bila mrahaba kwa malengo yaliyokusudiwa. Hii haikupi wewe, au mtu mwingine, haki ya kutoa kibali kwa mtu mwingine au kuhamisha haki zako kwa mtu wa tatu.
3.3. Unawajibika mwenyewe kuhakikisha kuwa;
3.3.1. Unaruhusiwa kisheria kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni; na
3.3.2. Madereva Wateule wanaofanya kazi kwa kwa niaba yako wanaruhusiwa kisheria kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni.
3.4. Bila kuathiri kipengele cha {3.3}, haki ya Dereva kufikia Jukwaa la Bolt kupitia – na, pale itakapohusika, kutimiza – fursa za kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni imetolewa pale tu:
3.4.1. kwa kipindi ambacho Dereva anaruhusiwa kisheria kutoa au kutimiza Huduma za Usafiri Mtandaoni. Hivyo, hii haki ya kufikia:
3.4.1.1. haitakuwepo hadi utakapokuwa umewapatia Bolt nyaraka sahihi zinazohitajika kuhakikisha ustahiki wa Dereva kisheria kutoa au kutimiza Huduma za Usafiri Mtandaoni katika soko husika (ikiwemo, pale inapohitajika, uthibitisho wa haki ya Dereva kufanya kazi);

3.4.1.2. itaisha mara moja endapo Dereva hatakuwa na kibali cha kutoa au kutimiza huduma husika au endapo Bolt itashindwa kuthibitisha kuwa Dereva anaruhusiwa kisheria kutoa huduma husika.
3.4.2. kwa kipindi ambacho utambulisho sahihi wa picha wa Dereva utakuwa umewasilishwa Bolt, kuhakikisha kuwa Dereva anaweza kutambulika wazi na Watumiaji kwa sababu za kiusalama;
3.4.3. kwa kipindi ambacho Dereva anaweza kuthibitisha utambulisho na/au utambulisho wa kuingia, kuzuia ufikiaji usioidhinishwa;
3.4.4. kuhusiana na kufikia Kitengo chochote kwenye Jukwaa, isipokuwa kwa Dereva kutimiza matakwa ya Kitengo, kama yapo {angalia kipengele cha 5.21} kwa ajili ya taarifa zaidi;
3.4.5. (wakati wewe ni Dereva) kuhusu utoaji wa Huduma ya Usafiri Mtandaoni kwa malipo ya pesa taslimu, kwa kipindi kile tu ambacho Salio la Akaunti yako ni kubwa kuliko kiasi kama inavyoonekana kwenye Programu ya Dereva (angalia kipengele cha {5.24} kwa taarifa zaidi).
3.4.6. kwa vipindi ambavyo matumizi ya Jukwaa la Bolt hayatasababisha uharibifu mkubwa kwenye ubora wake au uimara.
3.5. Kwa faida ya kuzuia ufikiaji usioidhinishwa, Bolt mara kwa mara inaweza:
3.5.1. kuhitaji nyaraka kadri itakavyoona inafaa ili kuhakiki kama Huduma za Usafiri zinaweza kufanyika kihalali; na
3.5.2. kuhitaji Watumiaji kuhakiki utambulisho wao na/au taarifa za kuingia kwenye Jukwaa.

**4. Taarifa zinazowasilishwa kwenye Jukwaa la Bolt**
4.1. Unapaswa kuhakikisha kwamba taarifa zote unawasilisha, au unazopanga kuziwasilisha, kwa Bolt kuhusiana na matumizi ya Jukwaa la Bolt, kuwa sahihi muda wote, ikiwemo (pale inapohitajika) jina lako, taarifa za mawasiliano, utambuzi wa picha, anwani, taarifa za kampuni, na hali ya usajili wa kikodi. Unawajibika pia kuboresha au kuondoa taarifa zozote ambazo sio sahihi au hazihitajiki tena.
4.2. Unawajibika wewe mwenyewe kuhakikisha kuwa taarifa zote na maudhui uliyowasilisha au ulizopandisha kwenye Jukwaa la Bolt (au Dereva Aliyeteuliwa) ni halali. Bolt inabaki na haki ya kuondoa maudhui yasiyo halali kutoka kwenye Jukwaa la Bolt muda wowote, ambayo inaweza kutokea bila taarifa ya awali. Endapo hii ikitokea, utakuwa na haki ya kupinga kulingana na kipengele cha {16.8}.
4.3. tafadhali tambua kuwa Bolt inaweza, baada ya kutoa onyo la awali, ikasitisha kufanyia kazi pingamizi ikiwa itaonekana kuwa malalamiko yasiyo ya msingi yatakuwa yameletwa mara kwa mara, kwa kuangalia uwingi wake, kiwango, ubaya, na kwa nia mbaya.

**5. Huduma za Usafiri Mtandaoni**
Muhtasari
5.1. Kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa, Madereva wanaweza kufikia Jukwaa la Bolt ili kupitia maombi ya Huduma za Usafiri wa Mtandaoni yaliyofanywa na Wateja na kuweza kuthibitisha utayari wao kutimiza maombi hayo.
5.2. Wateja wanaweza kuomba Huduma za Usafiri Mtandaoni kutolewa mara moja, au pale inapohitajika, kwa muda maalum.
5.3. Wateja wanapaswa kuthibitisha mapema kupitia Jukwaa la Bolt kama watalipia kwa ajili ya Huduma za Usafiri Mtandaoni:
5.3.1. kupitia kwenye Jukwaa la Bolt (ambapo Bolt itapanga kukusanya malipo stahiki kwa Mtoa Huduma kama wakala wake, kwa mujibu wa kipengele cha {7})
5.3.2. kwa pesa taslimu (kwa kumlipa Dereva husika, anayekusanya malipo kwa niaba ya Mtoa Huduma).

5.4. Bolt haithibiti Wateja au Wasafiri na, kwa hivyo:
5.4.1. Bolt haikuhakikishii uwepo wa fursa ya kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni; na
5.4.2. Bolt haitawajibika kwa kutokutenda au kutokutenda kwa Wateja au Wasafiri.

Maombi ya Huduma ya Usafiri wa Mtandaoni

5.5. Kuhusu maombi ya Huduma ya Usafiri Mtandaoni yaliyofanywa na Wateja, Bolt, ikisimama kama wakala wa Watoa Huduma kwa mujibu wa kipengele cha {7}:
5.5.1. kuamua makadirio ya nauli kwa ajili ya Huduma za Usafiri zitakazokubaliwa baina ya Wateja na Watoa Huduma, kwa kuzingatia:
5.5.1.1. njia na muda wa Huduma ya Usafiri Mtandaoni iliyoombwa;
5.5.1.2. (pale inapohusika) aina ya huduma iliyoombwa na Mteja;
5.5.1.3. (pale inapohusika) endapo Mteja ameomba kuchukuliwa haraka au ameomba kuchukuliwa kwa muda uliopangwa; na
5.5.1.4. sababu nyingine za kisoko kama vile upatikanaji na uhitaji wa Madereva.
5.5.2. kulingana na vipengele {5.6}, {5.7} na {5.8}, kuwakaribisha Madereva waliopo karibu sana na eneo la kuchukulia kuonyesha utayari wao kutoa Huduma ya Usafiri Mtandaoni, kwa kuzingatia (kwa madhumuni ya kuamua mpangilio na/au muda wa maombi hayo):
5.5.2.1. sababu zilizoainishwa katika kipengele cha {5.5.1};
5.5.2.2. (pale inapokuwepo) ombi la Mteja kwa gari husika; na
5.5.2.3. sababu nyingine zinazolenga kuharakisha mpangilio unaowezekana wa Huduma za Usafiri wa Mtandaoni, ikiwemo kadirio la muda wa Madereva kufika kwenye eneo la kuchukulia na pia endapo Madereva wanatoa Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa muda huo.
5.6. Katika baadhi ya maeneo yenye uhitaji mkubwa na idadi kubwa wa watumiaji wa mtandaoni, kama viwanja vya ndege, Bolt inaweza kutekeleza mfumo wa foleni wa “wa kwanza kuingia, wa kwanza kutoka” katika kuwaalika Madereva kuonesha utayari wao kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni. Endapo mfumo huo wa foleni utakuwa umetumika, itaoneshwa kwa Madereva kwenye Mfumo wa Dereva.
5.7. Ili kuharakisha upangaji wa Huduma za Usafiri Mtandaoni na kupunguza chaguzi zisizofaa, Bolt inaweza kuzingatia mazingira ambapo kuna mahusiano hasi, mrejesho au malalamiko yaliyowahi kutokea baina ya Mteja husika na Dereva husika.
5.8. Pale inapowezekana, Madereva wanaweza kurekebisha makaribisho wanayoyapokea kwa kuweka vichujio na vigezo ikiwemo vipengele vya bei vinavyopendekezwa au umbali kutoka maeneo ya kuchukuliwa. Uwepo wa taarifa hizi utaonyeshwa kwa Madereva katika Programu ya Dereva.
5.9. Pale Dereva anapoalikwa kupitia Programu ya Dereva kuthibitisha utayari wake kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni, Programu ya Dereva utaonesha taarifa zifuatazo katika hatua mbalimbali za safari:
5.9.1. nauli husika;
5.9.2. eneo la kupokelea lililoombwa;
5.9.3. kikomo cha safari kilichoombwa;
5.9.4. muda uliopangwa wa kupokelea (kama kupokea sio kwa uharaka); na
5.9.5. endapo Mteja atalipia Huduma za Usafiri Mtandaoni kupitia Jukwaa la Bolt au kwa pesa taslimu.
5.10. Baada ya Dereva kuonesha utayari wake kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni, Mteja husika;
5.10.1. (kulingana na maombi yao) atategemea Dereva kuelekea kwenye eno la kupokelea bila kuchelewa pasipo na sababu, au, pale inapohusika, kufika kwa muda stahiki; na
5.10.2. anakubali kukulipa Ada ya Kughahiri safari kulingana na vipengele vya {5.16} na {5.17}.
5.11. Kwa kufikia Jukwaa la Bolt kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa, unakubali kuwa

makubaliano yoyote ya kutoa Huduma ya Usafiri Mtandaoni baina yako na Wateja yatakuwa yamefanyika baada ya Dereva husika kuonesha nia yake ya kukamilisha Huduma za Usafiri Mtandaoni kupitia Programu ya Dereva.

5.12. Endapo Huduma ya Usafiri Mtandaoni imeanza, Mteja atakubali kukulipa:

5.12.1. Nauli, kama ilivyoonesha kwenye Programu ya Dereva kabla ya kuanza kwa Huduma ya Usafiri Mtandaoni; na

5.12.2. (kama inahusika) Ada ya Usafi, kwa mujibu wa vipengele vya {5.18} na {5.19}.

5.13. Wewe, na Dereva Aliyeteuliwa anayefanya kwa niaba yako, anaweza kukataa au kugoma kukuingiza kwenye makubaliano kwa ajili ya Huduma ya Usafiri Mtandaoni na Mteja yeyote kwa muda wowote, endapo tu kuna:

5.13.1. mazuio yanayohusiana na hatari za kiusalama na Tabia ya Kibaguzi kama ilivyoorodheshwa kwenye vipengele vya {10.2.1} na {10.2.2}; na

5.13.2. katazo kuhusu kukatisha Huduma za Usafiri baada ya kuthibitisha utayari wa kuzikamilisha, kama ilivyoainishwa kwenye kipengele {10.3.1}, ambalo linalenga kuzuia usumbufu uliokithiri au unaoendelea kwenye mpango wa Huduma za Usafiri Mtandaoni na Watumiaji na kwenye kulinganisha Wateja waliotayari na Watoa Huduma na Bolt (kama ilivyoelezewa katika kipengele cha {5}).

5.14. Pale Huduma za Usafiri Mtandaoni zinapokuwa zimehitimishwa (au zimekatishwa), Nauli stahiki itahesabiwa kwa mujibu wa msingi wa kiasi kilichooneshwa kwenye Programu ya Dereva kabla ya kuanza kwa Huduma ya Usafiri Mtandaoni.

5.15. kwa kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni, unakubaliana na Bolt kwamba hutaomba bila utaratibu au udanganyifu, au kuruhusu wengine kuomba, malipo ya nyongeza kutoka kwa Wateja au Wasafiri kuhusiana na Huduma za Usafiri Mtandaoni zinazokinzana na vigezo vya makubaliano na wao. Hii inajumuisha maombi kwa Wasafiri kulipia Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa pesa taslimu wakati ilikubaliwa awali kuwa Huduma za Usafiri Mtandaoni zitalipiwa kwa njia ya Jukwaa la Bolt na malipo kukusanywa na bolt kwa niaba yako.

5.16. Unakubali kuwa Ada ya Kusitisha iliyopo unayoweza kumtoza Mteja, kama Mteja akisitisha maombi yake (au akishindwa kuingia kwenye makubaliano) kwa ajili ya Huduma za Usafiri Mtandaoni baada ya kuisha kwa Muda wa Kusubiri, kiasi hicho itakuwa ni kile kilichooneshwa kwenye Jukwaa la Bolt kwa kwa aina ya huduma, kulingana na kipengele cha {5.17}.

5.17. Jukumu la Bolt kukusanya Ada ya Kusitisha itaendana na wewe kuwa na nia thabiti ya kuingia kwenye makubaliano ya kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni. Bolt haitakusanya Ada ya Kusitisha kwa niaba yako katika mazingira ambayo itaonekana kuwa hakukuwa na nia thabiti (kwa mfano, hakukuwa na jitihada Madhubuti zilizofanywa na Dereva kufika kwenye eneo la kupokelea kwa muda muafaka).

Ada za Usafi

5.18. Unaweza kumtoza Mteja Ada ya Usafi kama gari litachafuliwa Msafiri wakati wa kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni iliyoombwa na Mteja. Kwa ajili ya hili, unaiteua Bolt ikusanye hadi shilingi za Kitanzania Elfu Kumi (TZS. 10,000) kwa niaba yako, chini ya kipengele cha {5.19}. Katika mazingira haya, unapaswa kututaarifu mapema kuwa Ada ya Usafi inatakiwa kulipwa kupitia Jukwaa la Bolt au kwa kuwasiliana na Timu ya Usaidizi na kutoa risiti inayofuata matakwa ya kodi kwa ajili ya Ada ya Usafi. Kwa uelewa zaidi,hii haikuzuii kutaka kiasi cha ziada moja kwa moja kutoka kwa Mteja, kwa mfano pale unapotokea uharibifu makubwa, na ni halali kufanya hivyo. Unawajibika kuhakikisha kuwa chombo chako kimekatiwa bima ili kupunguza madhara ya uharibifu kama huo.

5.19. Bolt haitakusanya Ada ya Usafi kwa niaba yako kama utashindwa kutoa ushahidi wa kutosha kuwa gari lako lilichafuliwa na Msafiri husika, au endapo kutakuwa na ucheleweshwaji

wa taarifa kuhusu tukio husika. Tunapendekeza kuwa upate ushahidi wa picha na uwasilishe taarifa sahihi kwenye Timu yetu ya Usaidizi mapema iwezekanavyo, pale itakapokuwa salama kufanya hivyo.

Namna ya kukusanya malipo

5.20. Pale ambapo Mteja amekubali kufanya malipo kwa njia ya Jukwaa la Bolt, Bolt itakusanya kiasi unachostahili kulipwa kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa na kuituma kwako kwa kujibu wa kipengele cha {9}. Endapo Mteja amekubali kulipia Huduma za Usafiri kwa pesa taslimu, unawajibika kukusanya malipo hayo. Bolt haiwajibiki kukusanya au kurejesha malipo yoyote ya pesa taslimu kwa niaba yako.

Ufikiaji wa Makundi

5.21. Bolt inaweza kutengeneza Makundi mbalimbali za huduma katika soko ili kuoanisha: (i) Watoa Huduma kuwa na uwezo wa kukamilisha huduma kwa kulingana na kundi husika, na (ii) Wateja wanaochagua huduma inayotolewa kulingana na Aina husika. Kwa mfano, kama ‘gari inayotumia umeme’ ipo, Bolt inaweza kulenga kuwaunganisha Wateja kwa Watoa Huduma wenye wanaotumia gari inayotumia umeme. Makundi ya huduma yanaweza pia kuonyesha aina ya huduma, kama vile Huduma za Usafirishaji (tazama kipengele {5.28}).

5.22. Makundi yaliyopo kwa Dereva yatategemea mambo husika kulingana na kila aina na uhitaji wake sokoni (kwa mfano, Dereva ni lazima kutumia gari la umeme ili aweze kufikia Kundi la gari linalotumia umeme). Haki ya Dereva kufikia Makundi husika itakoma endapo Dereva atakuwa hajafikia matakwa ya Kundihusika (tazama kipengele {3.4.4})

5.23. Kwa taarifa zaidi kuhusiana na Makundi yaliyopo kwenye soko husika, tafadhali wasiliana na timu yetu ya usaidizi.

Kufikia Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa pesa taslimu

5.24. Ili kuzuia wewe kulipwa kiasi kisicholipwa kupita kiasi kulipwa kwako na Bolt, haki yako kufikia na kupitia fursa za kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni zinzolipiwa na Wateja kwa pesa taslimu inatolewa kwako pale tu endapo Salio la Akaunti yako halitapungua kiasi ambacho kitakuwa kimeonyeshwa kwenye Programu ya Dereva (tazama kipengele {3.4.5})

5.25. Kama hutotaka malipo ya Huduma za Usafiri Mtandaoni yafanyike kwa pesa taslimu, tunaweza (pale inapowezekana) kuzuia pale utakapoomba. Tafadhali wasiliana na timu yetu ya usaidizi kupanga hili. Kuzuia malipo ya pesa taslimu inaweza kukupunguzia fursa za kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni.

Ofa

5.26. Bolt inaweza, kwa hiari wake, inaweza kutoa Ofa maalum kwa Watoa Huduma ambapo Bolt itatoa faida kwa matumizi yao kwenye Jukwaa la Bolt.

5.27. Pale Ofa inapotolewa na Bolt kwa Watoa Huduma:

5.27.1. Kupokea faida kutategemea kukamilika kwa mahitaji husika kwenye ofa husika.

5.27.2. Ofa itaendana na kukidhi Masharti ya Jukwaa. Bolt inabaki na haki ya kuzuia faida ya ofa pale ambapo kutakuwa na uvunjwaji wa Masharti ya Jukwaa, ikiwemo pale tabia za Dereva zitaonesha uhusikaji kwenye Kitendo cha Udanganyifu kilichopigwa marufuku.

5.27.3. Kufikia Jukwaa la Bolt haitakuwa lazima ushiriki au umalizie punguzo yoyote.

5.27.4. Unakubali kuwa Bolt inaweza, pale inapopatikana, kutumia thamani ya punguzo kwa kupunguza Ada inayolipwa kwako na Bolt. Hii haitapunguza jumla ya thamani ya punguzo kwako.

Huduma za Usafirishaji

5.28. Bolt inawezesha Huduma za Usafirishaji iwepo kwa Watumiaji, Mteja anaweza kuomba usafirishaji wa bidhaa kutoka eneo la kupokelea hadi sehemu ya hitimisho bila usafirishaji wa Abiria. Madereva wanapaswa kuchagua kupokea maombi kwa ajili ya kukamilisha Huduma za Usafirishaji kwa niaba yako.

5.29. Bolt inakataza waziwazi Wateja kutokupanga usafirishaji wa bidhaa zifuatazo kupitia Jukwaa la Bolt:
5.29.1. vitu vyenye uzito wa zaidi ya kilo kumi na tano (15);
5.29.2. pesa taslimu (pamoja na pesa zozote za kigeni), kadi za malipo, dhamana, au vocha za zawadi;
5.29.3. silaha za moto na vifaa vyake, risasi, silaha za mkono au silaha za jadi, vifaa vingine vilivyotengenezwa mahususi kwa ajili ya kujeruhi na kujilinda (mfano vifundo, jambia ) vilipuzi, vinavyoweza kuwaka, mionzi, sumu, au bidhaa nyingine hatarishi;
5.29.4. vifaa vinavyoweza kuwaka, mionzi, sumu, au vifaa vya hatari vinavyofanana na hivyo;
5.29.5. chakula na vinywaji (pamoja na vilevi/pombe);
5.29.6. Wanyama, binadamu na viumbe vingine vilivyo hai au visivyo hai, pamoja na sehemu zake, mabaki, vimiminika au vitu vinavyotokana na wanyama, binadamu au viumbe vingine.
5.29.7. madawa ya kulevya, dawa, au vifaa vya matibabu;
5.29.8. bidhaa zenye thamani zaidi ya Shilingi za Kitanzania Laki Tatu;
5.29.9. vifaa ambavyo haviwezi kusafirishwa bila ya kuwa na leseni za nyongeza au vibali husika;
5.29.10. vifaa vikubwa au dhaifu ambavyo havifai kusafirishwa kwa gari; na
5.29.11. bidhaa haramu, zilizoibiwa au zisizoruhusiwa kisheria.
5.30. Unahimizwa kukataa na kusitisha Huduma zozote za Usafirishaji zinazohusu bidhaa zozote zilizoainishwa katika kipengele cha {5.29}. Katika mazingira hayo, tafadhali wasiliana na timu yetu ya usaidizi ili tuweze kupitia ufikiaji wa Mteja husika.
5.31. Unawajibika kuhakikisha kuwa Dereva anayefanya kwa niaba yako anaruhusiwa kisheria kukamilisha Huduma za kUsafirishaji na anatambua kuwa usafirishaji wa vitu haramu, au bidhaa zinazohitaji vibali muhimu, vinaweza kupelekea hatia ya jinai.
5.32. Kwa taarifa zaidi kuhusu Huduma za Usafirishaji, tafadhali wasiliana na timu yetu ya usaidizi.

**6. Kuteua Madereva wanaofanya kwa niaba yako**

Utangulizi

6.1. Pale inapopatikana, unaweza kusajili na kuteua watu kama Madereva kukamilisha Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa niaba yako (yaani ‘Madereva Wateule’), kwa mujibu wa kipengele hiki cha {6}.
6.2. Unawajibika kuhakikisha kuwa Madereva Wateule hawafanyi katika namna itakayokufanya wewe kuvunja Masharti haya ya Jukwaa. Hivyo unashauriwa kupitia vipengele hivi kwa umakini na kutathimini ustahili wa watu hao kabla ya kufanya uteuzi wowote.

Kufanya Uteuzi

6.3. ili kufanya uteuzi, unaweza kutumia anuani ya ufikiaji wa wavuti iliyotengenezwa na Bolt kwa ajili hiyo, au unaweza kuwasiliana na Bolt kupitia tanzania@bolt.eu kwa kutuma majina na taarifa za mawasiliano ya Madereva Wateule unaowependekeza. Bolt itathibitisha kama kuna uhitaji wa taarifa nyingine za ziada kulingana na soko/mahali ambapo uteuzi unafanyika.
6.4. Ingawa Bolt haina haki ya ujumla ya kukataa pendekezo la mtu yeyote mwenye sifa stahiki kama Dereva Aliyeteuliwa, mtu anaweza asisajiliwe kama Dereva Aliyeteuliwa kama Bolt imewahi kuvunja au kuzuia:
6.4.1. uhusiano wa mtu huyo kama Mtoa Huduma kwa uvunjaji wa wazi wa wajibu wake kwenye Masharti haya ya Jukwaa (pamoja na toleo lolote lililopita); au
6.4.2. Mtoa Huduma mwingine (kwa ujumla au kwa sehemu) kwa sababu ya matendo ya mtu huyo au kushindwa kufanya wakati akifanya kama Dereva Aliyeteuliwa wa Mtoa Huduma husika, ambayo ilisababisha uvunjwaji wa wazi wa wajibu wa Mtoa Huduma wa Masharti haya

ya Jukwaa (pamoja na toleo lolote liliopita).

6.5. Haki ya Dereva Aliyeteuliwa kufikia Jukwaa la Bolt ili kupitia fursa kwa ajili ya kukamilisha Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa niaba yako inatolewa tu kwa vipindi ambavyo Dereva Aliyeteuliwa atakuwa anastahili kisheria kukamilisha Huduma za Usafiri Mtandaoni (tazama kipenegele {3.4.1}). Unatakiwa kupanga kuipatia Bolt nakala za nyaraka ili kuhakiki kama Huduma za Usafiri Mtandaoni zinaweza kukamilishwa na Dereva (Madereva) Aliyeteuliwa, ikiwemo (pale inapohitajika), ushahidi wa haki ya kufanya kazi katika soko husika.

6.6. Kama utakuwa na maswali yoyote katika mchakato huu, tafadhali wasiliana na timu yetu ya usaidizi.

Masharti muhimu kuhusu Madereva Wateule

6.7. Unapomtumia Dereva Aliyeteuliwa, utaendelea kuwajibika kuhakikisha kuwa majukumu yako ndani Masharti haya ya Jukwaa yanafuatwa. Matendo yote na mapungufu ya Dereva Aliyeteuliwa yatachukuliwa kuwa kama ya kwako. Hivyo, ni wajibu wako kuhakikisha kuwa Dereva Aliyeteuliwa hakusababishii wewe kuvunja Masharti ya Jukwaa.

6.8. Unakubali kuwa unawajibika kikamilifu kwa yafuatayo kwa kila Dereva Aliyeteuliwa:

6.8.1. unakubali na kuandika masharti husika kati yako wewe na yeye, ikiwemo masharti yoyote yanayotakiwa chini ya sheria inayotumika;

6.8.2. kuwalipa malipo yao;

6.8.3. malipo ya Ada yanayopaswa kulipwa kwa Bolt (kulingana na kipengele cha {8})

6.8.4. kukidhi matakwa yote ya kisheria yatokananyo na uhusiano wao na wewe;

6.8.5. kuhakikisha kuwa taarifa zilizotolewa kwa Bolt kuhusu Dereva Aliyeteuliwa ni sahihi na zimesasishwa; na

6.8.6. maudhui yoyote yaliyopandishwa kwenye Jukwaa la Bolt na Dereva Aliyeteuliwa.

6.9. Kuhusu kila Dereva Aliyeteuliwa:

6.9.1. unaihakikishia Bolt kuwa una makubaliano halali na Dereva Aliyeteuliwa yanayomuwezesha kihalali kupitia, kukubali na kukamilisha Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa niaba yako; na

6.9.2. Unakubali kuwa Bolt inaweza kuwasiliana na Dereva Aliyeteuliwa moja kwa moja na mara kwa mara ili kuharakisha masuala yanayohusu haki ya kufikia (tazama kipengele {3.4}) na {3.5} uchunguzi kwenye tabia isiyo ya kawaida (tazama kipengele cha {11}).

6.10. Kwa madhumuni ya kuondoa shaka:

6.10.1. Isipokuwa kama inavyohitajika na vipengele {6.4}, {6.5}, na {6.9.1}, Bolt haiweki vizuizi vyovyote au matakwa kwenye mipango ya kibiashara iliyofanywa kati ya:

6.10.1.1. wewe na Madereva Wateule wako; au

6.10.1.2. Madereva Wateule wako; na

6.10.2. hakuna chochote ndani ya Masharti haya ya Jukwaa kinacholenga kuzuia Dereva Aliyeteuliwa kutoa huduma ya usafiri mtandaoni nje ya Jukwaa la Bolt.

**7. Jukumu la Bolt kama wakala wako**

7.1. Kwa kufikia Jukwaa la Bolt kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa:

7.1.1. unatupatia haki zako zote kwa ajili ya sisi kukidhi wajibu wetu katika Masharti ya Jukwaa kwa kipindi cha mahusiano yetu. Hii inajumuisha kutupatia haki - pale inapohusika, kututeua kuwa wakala wenye mamlaka - ya:

7.1.1.1. kukulinganisha wewe na Madereva Walioteuliwa na Wateja, kama ilivyoelezwa kwenye kipengele cha {5};

7.1.1.2. kukokotoa Nauli izote, ikiwemo makadirio ya Nauli na Malipo ya Ushuru yaliyopo, yanayolipiwa kwa Huduma za Usafiri Mtandaoni;

7.1.1.3. kukusanya Nauli, Ada za Kukatisha, na Ada za Usafi zinazopaswa kulipwa kwako na

Wateja na kutuma malipo hayo kwako; na

7.1.1.4. kutoa risiti na/au ankara kwa niaba yako.

7.2. Kuhusu kiasi kilichokusanywa, au kitakachokusanywa, na sisi kwa niaba yako kwa mujibu wa Masharti haya ya Mfumo, unakubali kuwa wajibu wa Mlipaji wa Malipo yanayotokana na mkataba wowote wa Huduma za Usafiri Mtandaoni yanachukuliwa kuwa yamekamilika pale malipo husika yanapokukuwa yamefanywa kwenye akaunti zetu za malipo.

7.3. Unakubali kutupatia taarifa zaidi tunazoweza kuhitaji, kwa ombi na mara kwa mara, ili kuiwezesha Bolt kutimiza wajibu kama wakala wako kwa ufasaha na kisheria katika soko/masoko husika kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa.

7.4. Bolt itatoa risiti na/au ankara (kama itakavyostahili) kwa niaba yako na kwa njia ya kieletroniki kuhusiana na kiasi kinachopaswa kulipwa kwako. Unakubali kuwa tunaweza kujumuisha katika risiti na ankara hizo taarifa zinazohusiana na Huduma za Usafiri Mtandaoni, ikiwa ni pamoja na mchanganuo wa ada zozote zinazotumika.

**8. Kamisheni**

8.1. Unapaswa kulipa Kamisheni kwa Bolt katika kiasi chote kinacholipwa kwako na Wateja kuhusiana na Huduma za Usafiri Mtandaoni, ikiwemo malipo taslimu, isipokuwa kwa Bidhaa zisizo na Kamisheni.

8.2. Kiwango cha mwanzo cha Kamisheni kitakachotumika kwako kitakuwa kile kilichoonyeshwa kwako kwa maandishi mara kabla ya kujisajili kama Mtoa Huduma kwenye Jukwaa la Bolt.

8.3. Tunaweza kufanya mabadiliko kwenye kiwango/viwango vya Kamisheni kitakachotumika kwako, mara kwa mara, kwa kutoa kiwango/viwango kipya kwako kwa maandishi angalau siku kumi na tano (15) kabla ya mabadiliko hayo kufanyika.

8.4. Wajibu wako kulipa Kamisheni kwa Bolt unatokea kwa wakati uleule ambapo kiasi ambacho kinachohusiana na Huduma za Usafiri Mtandaoni kinakuwa kinastahili kulipwa kwako. Viwango vyote vya Kamisheni vinavyokuhusu havijumuishi kodi yoyote inayotumika kwako, ikiwemo kodi ya ongezeko la thamani, isipokuwa kama imeelezwa tofauti.

8.5. Unakubali kuwa Bolt inaweza kukata Kamisheni mara moja, Pamoja na kiasi kingine kinachopaswa kulipwa kwa Bolt, kutoka kwenye malipo yanayokusanywa na Bolt kwa niaba yako pale ambapo malipo yamefanyika kwenye akaunti zetu za malipo.

8.6. Unakubali kwamba Bolt inaweza kukata kodi kutoka katika kiasi chochote kinachopaswa kulipwa kwako na Bolt kodi yoyote inayopaswa kukatwa kwa mujibu wa sheria au kanuni zozote zinazotumika

**9. Masharti yanayohusu malipo ikiwemo pale Bolt itatuma malipo kwako**

Salio la Akaunti na ratiba yetu ya malipo ya kawaida

9.1. Bolt itapanga kutuma malipo kwako kupitia Njia yako ya Malipo mara kwa mara kulingana na Salio la Akaunti yako, ambayo inakokotolewa (kwa mujibu wa masharti mengine kwenye kipengele hiki cha {9}) kama ifuatavyo:

9.1.1. Jumla ya:

9.1.1.1. malipo yaliyopangwa kukusanywa na Bolt kwa niaba yako kulingana na Masharti haya ya Jukwaa; na

9.1.1.2. (pale inapohusika, na kwa mujibu wa kipengele cha {5.27}) thamani ya ofa yoyote kama ilivyotolewa na Bolt ambazo ziko tayari kupokelewa na wewe;

9.1.2. Kupunguza:

9.1.2.1. Kamisheni zote na kiasi chochote kinachotakiwa kulipwa na wewe kwa Bolt kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa; na

9.1.2.2. Malipo yoyote yaliyopangwa kufanywa na wewe kwa Bolt kwa mujibu wa kipengele hiki cha {9}.
9.2. Endapo Salio la Akaunti yako liko chanya inapofika mwisho wa kila wiki ya kalenda utakuwa unastahili kupokea malipo (kwa mujibu wa kikomo kilichowekwa katika kipengele cha {9.3} na masharti mengine ya kipengele hiki cha {9}. Bolt itapanga kuhamisha kiasi cha Salio la Akaunti yako kwenda kwako kupitia Njia yako ya Malipo itakayokokotolewa kama ilivyo tarehe ya malipo.
9.3. Kwa nia mahsusi ya kupunguza tozo za uendeshaji kuhusiana na malipo, unakubali kuwa Bolt haitahitaji kukutuma Salio la Akaunti yako pale litakapokuwa dogo kuliko kikomo kilichowekwa kwenye Jukwaa la Bolt. Katika mazingira hayo, kiasi hicho kitatunzwa kama sehemu ya Salio la Akaunti yako na kitakuwa tayari kulipwa kwa atrehe nyingine pale kikomo kitakapokuwa kimezidi.
9.4. Iwapo Salio la Akaunti yako litafikia kiwango cha juu cha kiasi unachodaiwa na Bolt, utakuwa na deni kwa Bolt. Katika mazingira hayo, utapaswa kuhamisha malipo husika kwenda Bolt kupitia hamisho la kibenki, malipo ya pesa kwa simu au njia nyingine ya malipo iliyotolewa na Bolt sio zaidi ya siku ya kumi na tano (15) ya mwezi wa kalenda unaofuata, kwa kutumia taarifa za njia ya malipo ambayo tutakupatia kwa ajili hii.

Kuomba Malipo ya mapema

9.5. Pale inapopatikana, unaweza kuwa unastahili kuomba malipo ya vipato vyako kabla ya muda wa malipo wa kawaida kama ilivyoonyeshwa katika kipengele {9.1} kupitia Programu ya Dereva (‘Malipo ya Mapema’)
9.6. Maombi ya Malipo ya Mapema:
9.6.1. yanaweza kufanyika pale tu dhidi ya Salio la Akaunti iliyo chanya; na
9.6.2. pale inapokamilika, itapunguza kiasi kile unachostahili kulipwa katika ratiba ya malipo ya kawaida kama ilivyoonyeshwa katika kipengele cha {9.1}.
9.7. Kila Malipo ya Mapema yanaweza kuwa na ada, ambayo (kama ipo) itakuwa imeoneshwa kwako awali kwenye Programu ya Dereva. Kwa kuomba Malipo ya Mapema, unakubali kuwa ada stahiki zitakatwa kutoka kwenye Salio la Akaunti yako.

Njia yako ya Malipo

9.8. Unapaswa kuhakikisha kuwa taarifa zako ulizotoa kwetu kuhusiana na Njia ya Malipo inahusiana na akaunti ya benki ndani ya nchi (au njia nyingine ya akaunti ya malipo inayokubaliwa na Bolt) iliyoko kwenye jina lako na hakikisha zinakuwa sahihi zimesasishwa.
9.9. Pale unaposasisha taarifa zako za Njia ya Malipo, inaweza kuchukua siku kadhaa kwa mabadiliko ya kiutawala kuanza kutumika. Kwa hivyo, tunakushauri kuwa uboreshe taarifa zako za Njia ya Malipo haraka inavyowezekana.
9.10. Kama tutashindwa kutimiza wajibu wetu wa kufanya malipo unayostahili kwa sababu ya taarifa za Njia yako ya Malipo (au taarifa nyingine zilizotolewa kwetu) zitakuwa na makosa, zimepitwa na wakati au haziruhusiwi kwa namna yoyote ile na Masharti haya ya Jukwaa:
9.10.1. tutatunza malipo hayo kwa muda kwenye akaunti yetu kwa muda wa kikomo wa siku mia moja na themanini (180) za kalenda kuanzia tarehe ambayo malipo yalipaswa kufanyika kwa mara ya kwanza; na
9.10.2. Iwapo hautatupatia zilizosasishwa ndani ya kipindi hicho ambazo zitatuwezesha kukamilisha malipo, madai yako ya kiasi ambacho hakijalipwa yatapoteza uhalali.

Taarifa nyingine muhimu kuhusiana na malipo

9.11. Maelezo yoyote yanayoonyesha Salio la Akaunti yako na Bolt yanafanywa bila kuathiri kiasi chochote unachopaswa kulipa kwa kwa Bolt katika kipengele cha {14} (‘Deni lako’).
9.12. kwa kukubaliana na Masharti haya ya Jukwaa, unakubali kupokea risiti na ankara kutoka kwetu katika muundo wa kielektroniki.

9.13. Bolt haitawajibika kwa, na haitakuhakikishia, malipo yoyote yaliyofanywa na watu wengine. Hivyo basi, hatutawajibika kukulipa kiasi chochote ambacho tumeshindwa kukikusanya kwa niaba yako kwa sababu zilizo nje ya uwezo wa Bolt (mfano, endapo njia ya malipo ya mlipaji imeshindwa kufanya kazi). Hivyo, Huduma zote za Usafiri Mtandaoni unazitoa kwa hatari yako ya kifedha.
9.14. Inapotokea malipo yameshindikana, tutakupa msaada stahiki kutafuta/kurejesha kiasi ulichopaswa kulipwa kutoka kwa mlipaji husika. Kama Bolt itaweza kukusanya malipo hayo kwa niaba yako, tutaweka malipo hayo kwenye Akaunti yako ya Salio.
9.15. Malipo kwako, pamoja na huduma zinazohusiana, yanaweza kuingiliwa, kusitishwa, au kupunguzwa mara kwa mara kutokana na matengenezo au hitilafu za kiufundi.
9.16. Iwapo kutatokea malipo ya ziada kwako, au kosa lolote linalofanana na ukusanyaji au utozaji wa kimakosa:
9.16.1. unakubali kuwa Bolt inaweza kuchukua hatua stahiki kurekebisha kosa, ikiwemo kupunguza Salio la Akaunti au kupunguza kiasi chochote kilichohamishwa kimakosa kwako kutoka kwenye Akaunti ya Salio kwa baadae; na
9.16.2. isipokuwa kama kosa hilo litarekebishwa kwa namna nyingine, unakubali kurudisha malipo yoyote ya ziada kwa Bolt pale tutakapokutaarifu kuhusu kosa hilo (na kwa hali yoyote ndani ya siku saba (7) za kalenda baada ya taarifa).
9.17. Bolt inabaki na haki ya kukatisha, kusimamisha, kuzuia, au kukataa malipo kwako, au makusanyo kufanyika kwa niaba yako, kama Bolt ina sababu za msingi kuhisi kuwa malipo hayo au makusanyo yatakuwa ya kimakosa au ni kinyume na sheria, yanahusu Kitendo cha Udanganyifu kilichopigwa marufuku, au inahusu matumizi mengine ya Jukwaa la Bolt ambayo ni kinyume cha sheria, haramu au kimezuiliwa na vikwazo vya kimataifa.
9.18. Pale inapowezekana, Bolt itajaribu kuwasiliana na wewe mapema kukutaarifu kutokea kwa jambo lolote lililoelezwa kwenye vipengele {9.14} hadi {9.17} (kwa ujumla) na, pale inapohitajika, itajaribu kuyatatua, labda kama imezuiliwa kufanya hivyo na taratibu au matakwa ya kisheria, au pale Bolt itakapokuwa imeshauriwa na mamlaka sahihi, watoa huduma ya malipo, au mshauri wa kisheria kutokufanya hivyo.
9.19. Bolt watatuma taarifa muhimu kuhusu wewe na kazi zako za kiuchumi zinazofanyika kupitia Jukwaa la Bolt kwa mamlaka za kodi kama itahitajika kufanya hivyo kulingana na sheria za kodi. Unathibitisha na unakubali kuwa utoaji wa taarifa utafanyika kama sehemu ya wajibu wa kisheria wa Bolt.

**10. Marufuku ya jumla**
10.1. Usitumie, au kuruhusu matumizi ya, Jukwaa la Bolt kujihusisha na, au kwa sababu yoyote inayohusiana na:
10.1.1. kitendo chochote kinyume cha sheria au haramu - ikiwemo kushirikiana maudhui, taarifa, au bidhaa zilizozuiliwa kwenye sheria zilizopo, au kuchakata taarifa binafsi kusiko halali; au
10.1.2. vitendo vya udanganyifu vilivyopigwa marufuku.
10.2. Wakati wa Vipindi vyote vya Maombi ya Huduma, hutakiwi - na unapaswa kuhakikisha, kwa kila kipindi husika, kuwa kila Dereva Aliyeteuliwa ambaye ameonesha kuwa na nia ya kutimiza Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa niaba yako hatafanya yafuatayo:
10.2.1. kutengeneza mazingira ya hatari yasiyo ya lazima kwa Watumiaji wengine, ikiwemo:
10.2.1.1. kuendesha kinyume cha sheria za usalama barabarani au taratibu za usalama zilizotolewa na mamlaka za usimamizi;
10.2.1.2. kuwaweka Watumiaji wazi kwa silaha au vifaa vingine hatarishi bila ulazima;
10.2.1.3. kutumia magari ambayo sio salama kwa sababu ya hali mbaya; au

10.2.1.4. kutenda kwa namna nyingine katika hali ya kizembe ambayo haizingatii usalama wa Watumiaji wengine;
10.2.2. kujihusisha au kushawishi:
10.2.2.1. tabia ya hatari, ugomvi au inayotisha;
10.2.2.2. tabia yoyote ya Kibaguzi;
10.2.3. kusababisha wasiwasi mkubwa na usio wa lazima wa usalama au kukosa amani kwa Watumiaji wengine, ikiwemo:
10.2.3.1. mawasiliano yasiyohitajika au ushawishi wa ngono unaofanya wengine kukosa amani, usalama au kujisikia vibay;
10.2.3.2. kukaribisha au kuruhusu watu wasiojulikana kwa Wasafiri kuingia kwenye magari wakati wa Huduma za Usafiri Mtandaoni; au
10.2.3.3. kuwaweka watu wengine katika hali zisizofaa au zisizokubalika mara kwa mara, ikiwemo viti vichafu au harufu mbaya.
10.3. Utendaji sahihi wa Jukwaa la Bolt unategemea Watumiaji wote kutumia kwa 'nia njema' na kuwa na kuwajali wengine. Kwa sababu hiyo, hupaswi kutumia Jukwaa la Bolt, au kuruhusu matumizi yake, katika njia yoyote ambayo mara kwa mara inavuruga, inaingilia, au kuchelewesha Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa Watumiaji, au mlinganisho wa utayari kwa Wateja na Watoa Huduma kwa Bolt (kama ilivyoelezwa katika kipengele cha {5}), ikiwa ni pamoja na:
10.3.1. kukatisha Huduma za Usafiri Mtandaoni mara kwa mara baada ya kuthibitisha utayari wa kuzikamilisha;
10.3.2. kubaki kwenye 'mtandaoni' mara kwa mara kwenye Programu ya Dereva katika vipindi ambavyo haufanyi kazi;
10.3.3. kuchelewesha mara kwa mara kukatisha Huduma za Usafiri Mtandaoni baada ya kuamua kutokuzikamilisha;
10.3.4. kuwaomba Wateja kukatisha Huduma za Usafiri Mtandaoni, badala ya wao kukatisha kwa usahihi kupitia Programu ya Dereva, baada ya kuamua kutokuzikamilisha; au
10.3.5. (bila kuathiri haki yako, na haki ya Madereva Walioteuliwa, kukatisha au kukataa huduma kama inavyoonyeshwa katika kipengele cha {5.13}) au kujihusisha kwa namna nyingine na Programu ya Dereva katika hali ambayo haiendani na uimara, lengo la nia njema kupitia, na pale inapohusika kutimiza, Maombi ya Huduma za Usafiri Mtandaoni.
10.4. unapaswa usitoe, au kuruhusu utoaji wa, taarifa yoyote kupitia Jukwaa la Bolt zinazochanganya, za uongo, kinyume cha sheria au haramu.
10.5. Haupaswi kuruhusu mtu yeyote kufikia Jukwaa la Bolt kwa kutumia taarifa ambazo haziendani na taarifa zilizotolewa kwa Bolt kwa mujibu wa vipengele {3.4.1} ('uwezo wa kisheria wa kutoa au kutekeleza huduma kwa mujibu wa sheria'), {3.4.2} ('utambulisho wa picha'), {4.1} ('taarifa binafsi'), au {6.5} ('taarifa kuhusu Madereva Walioteuliwa')
10.6. Haupaswi kujihusisha na, au kuruhusu, kujaribu:
10.6.1. kudanganya, kutumia isivyo sahihi, kuharibu, kukusanya taarifa yoyote iliyopo kwenye Jukwaa la Bolt;
10.6.2. kuharibu, kudanganya, au kuinglia mifumo ya usalama ya Jukwaa la Bolt;
10.6.3. kubadilisha, kuvunja, kutawanya, kugeuza ufundi au kujaribu kwa namna yoyote kupata namba ya chanzo ya sehemu yoyote ya Jukwaa la Bolt;
10.6.4. kufikia Jukwaa la Bolt kupitia njia yoyote tofauti na zile zilizotolewa na kuruhusiwa kupitia mifumo rasmi ya Bolt, tovuti au kwa njia nyingine yeyote; au
10.6.5. kujihusisha na matumizi mengine ya Jukwaa la Bolt ambayo yanaweza kuwa na madhara makubwa hasi katika ubora au hadhi ya Mfumo.
10.7. Kwa madhumuni ya kuepuka utata, katazo la Tabia ya Kibaguzi lililopo katika kipengele

cha {10.2.2} halizuii haki yako, au haki ya Dereva Aliyeteuliwa, kukataa maombi au kutokujihusisha na mwingiliano kwa sababu za msingi na za kisheria.
10.8. Bolt haina sera ya uvumilivu kwa tabia ya ugomvi, vitisho au udanganyifu. Haupaswi, na usiruhusu Madereva Walioteuliwa, kuwatisha, kuwaogopesha, kuwalaghai kijanja au kuwaudhi wafanyakazi wowote, washirika au mawakala wa Bolt.

**11. Uchunguzi kuhusu tabia isiyo ya kawaida**
11.1. Endapo Bolt itapata taarifa inayoonesha uvunjifu wa wazi wa Masharti haya ya Jukwaa, unapaswa kujiandaa kutoa ushirikiano wa kutosha katika uchunguzi wa msingi wa Bolt bila kuchelewa.
11.2. Unakubali kuwa Bolt inaweza kuomba mrejesho kutoka kwa Watumiaji ili kusaidia kutambua ukiukwaji wa Masharti ya Jukwaa.
11.3. Bolt inayo haki ya kutoa taarifa juu ya vitendo vyovyote visivyo halali, ambavyo sio vya kawaida au vyenye kutia mashaka kwenye vyombo husika vya dola au mamlaka za usimamizi bila kukupatia taarifa au kutoa taarifa kwa mtu mwingine.
11.4. Bolt inaweza kuhitajika kutoa taarifa za siri kwa mujibu wa na sheria husika, amri ya mahakama au vyombo vya uchunguzi.

**12. Jinsi gani upatikanaji wa Jukwaa la Bolt unavyoweza kusitishwa kwa muda**
12.1. Bolt ina mamlaka, kwa utekelezaji wa mara moja, kusitisha au kuzuia kwa muda, kwa sehemu au kwa jumla, dhidi ya sehemu yoyote ya Jukwaa la Bolt inayohusiana na akaunti yako:
12.1.1. endapo kutakuwepo na kutokutimiza wajibu wako katikaMasharti ya Jukwaa;
12.1.2. pale Bolt itakuwa inafanya uchunguzi kuhusu:
12.1.2.1. wajibu wa Bolt wa kisheria au wa kiusimamizi; au
12.1.2.2. ukiukaji unaoshukiwa wa Masharti haya ya Jukwaa.
ambapo katika hali hiyo, upatikanaji husika utasitishwa kwa muda wa uchunguzi pekee;
12.1.3. endapo wewe na/au Madereva wako Wateule wameshindwa kuhakiki utambulisho wao na/au taarifa za kuingia kwenye Jukwaa;
12.1.4. endapo Bolt itahitaji kufanya mabadiliko ili kufuata matakwa ya sheria au kanuni;
12.1.5. kupambana na changamoto za ghafla za kiufundi, mabadiliko, au maboresho; au
12.1.6. endapo Bolt inahitajika kuchukua taadhari za haraka kujilinda dhidi ya:
12.1.6.1. hatari ya ghafla kwa Watumiaji;
12.1.6.2. hatari za usalama mtandaoni (ikiwemo programu hasidi, barua taka, au ukiukaji wa usalama wa data);
12.1.6.3. kitendo kinachoshukiwa kuwa kinyume na sheria au haramu; au
12.1.6.4. madhara mengine makubwa kwenye uadilifu au sifa za Jukwaa la Bolt.
12.2. Bolt itajaribu kuwasiliana nawe kabla ya zuio hilo, labda kama kuna jambo la haraka, dharura, au sababu nyingine ya msingi, ikiwemo:
12.2.1. masuala ya afya na usalama;
12.2.2. uvunjifu uliokithiri au unaojirudia waMasharti haya ya Jukwaa; au
12.2.3. endapo tutashindwa, au tumeshauriwa kutokufanya hivyo, kwa sababu za kiusimamizi au za kisheria.
12.3. Wakati umezuiliwa au umesimamishwa, utaweza (pale itakapopatikana) kufikia taarifa za kihistoria kuhusu Huduma za Usafiri Mtandaoni ambazo umetoa kupitia Jukwaa la Bolt.
12.4. Endapo Bolt imekusimamisha kulifikia Jukwaa la Bolt, unaweza kuwasilisha lalamiko au kuomba marejeo ya uamuzi kwa mujibu wa kanuni zetu za ndani za uendeshaji wa malalamiko (tazama kipengele {16.8})

**13. Namna uhusiano wetu unaweza kukoma**

13.1. Unaweza kusitisha uhusiano wako na Bolt katika Masharti haya ya Jukwaa mara moja na wakati wowote kwa kutoa taarifa husika kwa maandishi.

13.2. Bolt inaweza kusitisha uhisiano wake na wewe, moja kwa moja au kwa sehemu husika au aina ya kufikia, kama ifuatavyo:

13.2.1. kwa kukupatia notisi husika angalu siku thelasini {30}, pamoja na sababu za Bolt kufanya hivyo; au

13.2.2. mara moja, kwa kukupatia notisi husika, endapo:

13.2.2.1. kuna sheria mpya, kanuni, au wajibu umeanza kutumika (au mazingira kama hayo yaliyo nje ya uwezo wa Bolt) inayoilazimu Bolt kusitisha utendaji wa Jukwaa la Bolt mara moja au kwa notisi ya siku zisizopungua thelathini (30);

13.2.2.2. Bolt inatimiza haki yake ya kusitisha kwa sababu ya lazima kwa mujibu wa sheria ya nchi;

13.2.2.3. kuna uvunjifu mkubwa wa Masharti haya ya Jukwaa; au

13.2.2.4. kuna uvunjifu unaojirudia wa Masharti haya ya JUkwaa.

13.3. pale itakapohitajika kufanya hivyo, Bolt itakupatia maelezo ya sababu za sitisho lolote kwa mujibu wa kipengele {13.2}, isipokuwa pale ambapo tutakuwa tumeshindwa kufanya hivyo au tumeshauriwa tusifanye hivyo kwa ajili ya sababu za kisheria au kiusimamizi. Kutokuwepo kwa maelezo ya sababu hakutaathiri uhalali wa notisi ya sitisho ambayo itakuwa imetolewa kwa taratibu sahihi na Bolt.

13.4. Baada ya kusitisha Masharti haya ya Jukwaa:

13.4.1. kwa ujumla, wewe na Madereva wako Wateuliwa hamtakuwa na haki ya kuingia kwenye Jukwaa la Bolt; au

13.4.2. kuhusiana na hudumafulani au kufikia sehemu fulani, wewe na/au Madereva wako Wateuliwa husika (inapohitajika) hamtakuwa na haki ya kufikia sehemu za Jukwaa la Bolt zenye huduma hiyo.

13.5. Kusitishwa kwa Masharti haya ya Jukwaa haitaathiri haki yoyote iliyokuwepo au wajibu uliokuwepo kabla ya kusitisha.

13.6. Endapo Bolt itasitisha kuingia kwako kwenye Jukwaa la Bolt, unaweza kuwasilisha lalamiko au kuomba marejeo ya uamuzi kwa mujibu wa kanuni za ndani za kupokea malalamiko (tazama kipengele {16.8}).

13.7. Ili kuondoa mashaka yoyote, vipengele vinavyofuata vya Masharti ha ya Jukwaa vitaendelea kutumika kwa wakati wote ikiwemo baada ya kusitisha uhusiano wetu wote au kwa sehemu: {7} (wigo wa jukumu la Bolt kama wakala wako), {8} (Kamisheni), {9} (malipo), {14} (uwajibikaji wako), {16} (haki miliki, notisi, migogoro, washirika wetu, kodi, tasfiri na mamlaka) na {17} (faharasa ya maneno yaliyofafanuliwa).

**14. Uwajibikaji wako**

14.1. Kwa kiwango kilichoruhusiwa kisheria, unakubali kufidia na kuirudishia Bolt madai, hasara, madeni, na gharama (ikiwa na Pamoja na gharama za washauri wa kitaalamu wa Bolt na mawakala wa utekelezaji) zilizoingiwa kwa sababu ya matumizi yako ya Jukwaa la Bolt, ikiwemo na zinazohusu:

14.1.1. uvunjifu wowote wa wajibu wako kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa;

14.1.2. uharibifu wa mali au hasara ya pesa;

14.1.3. kusababisha hasara, biashara, mapato, mikataba, mawasiliano, heshima ya kibiashara, hadhi, au akiba iliyotarajiwa;

14.1.4. hasara yoyote inayotokana na kuingilia au matumizi ya Jukwaa la Bolt;

14.1.5. kupoteza, kuharibu au taarifa zisizo sahihi;

14.1.6. aina nyingine yoyote ya hasara isiyo ya moja kwa moja au hasara ya matokeo au uharibifu (kwa mfano, hasara ambazo isingekuwa rahisi kuzifikiria mwanzoni mwa uhusiano wetu);
14.1.7. tuhuma yoyote kwamba taarifa zozote zilizowasilishwa Bolt au zilizosambazwa kupitia Jukwaa la Bolt:
14.1.7.1. inavunja haki miliki ya mtu mwingine; au
14.1.7.2. inavunja sheria yoyote au kanuni;
14.1.8. umiliki, matumizi, matengenezo, au uendeshaji wa gari;
14.1.9. kushindwa kwako au Dereva yeyote Aliyeteuliwa kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni;
14.1.10. matendo au mapungufu ya Madereva Wateuliwa; na/au
14.1.11. uhusika wako na Madereva Wateuliwa.
14.2. Isipokuwa pale itakuwa imetajwa kivingine kwenye Masharti haya ya Jukwaa, unakubali kulipa kiasi chochote kinachopaswa kulipwa kwa Bolt mara tu utakapohitajika kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa (ikiwemo hasara yoyote iliyolipwa, malipo ya ziada, riba, au gharama za utekelezaji). Bolt inaweza, pale inapohitajika, kurejesha kiasi hicho kwa kukikata kutoka kwenye kiasi chochote kilicokusanywa kwa niaba yako au kwa kutoa Ankara tofauti.
14.3. Malipo yako yoyote yatakayofanywa kwa kuchelewa kwa Bolt kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa yatalipwa pamoja na riba kwenye kiasi ambacho hakijalipwa, endapo imewekwa na Bolt, ambayo itakokotolewa kwa 2% (asilimia mbili) ya kiasi ambacho hakijalipwa kwa kila mwezi.

**15. Uwajibikaji wetu**
15.1. Bolt haitawajibika kwako kwa hasara yoyote, uharibifu, gharama, au malalamiko yatokanayo au yanayohusiana na:
15.1.1. matumizi yako ya Jukwaa la Bolt, au matumizi ya Jukwaa la Bolt na Dereva Aliyeteuliwa;
15.1.2. kutokupatikana, kuvurugika, au utendaji mbaya wa Jukwaa la Bolt;
15.1.3. matendo au mapungufu ya Mtumiaji yeyote wa Jukwaa la Bolt;
15.1.4. tovuti, maudhui, mifumo, au huduma (ikiwemo huduma za malipo) ambazo hazimilikiwi, kusimamiwa au kuendeshwa na Bolt, ikiambatana na ucheleweshwaji au makosa yanayosababishwa nazo;
15.1.5. utoaji wa taarifa zisizo sahihi au zilizopitwa na wakati ulizotoa Bolt;
15.1.6. uchelewaji wa mifumo ya malipo iliyopo nje ya uwezo wa Bolt (kwa mfano, ucheleweshwaji unaosababishwa na mtoa huduma ya malipo mwingine); au
15.1.7. kuingia kwenye Jukwaa la Bolt kusikoruhusiwa kwa kutumia taarifa zako za kuingia kwenye Jukwaa au mtu mwingine anayefanya kwa niaba yako.
15.2. Kuondolewa kwa wajibu katika kipengele cha {15.1} kunajumuisha, bila kikomo, kutohusika kwa chochote kwenye aina yoyote ya hasara au uharibifu, iwe ya moja kwa moja au kwa namna nyingine:
15.2.1. uharibifu wa mali au hasara ya fedha;
15.2.2. kutopata faida, hasara ya biashara, mikataba, mawasiliano, sifa ya biashara, hadhi, au akiba tarajiwa;
15.2.3. hasara yoyote itokanayo na muingiliano au matumizi ya Jukwaa la Bolt;
15.2.4. upotevu wa taarifa, uharibifu wa taarifa au taarifa zisizo sahihi; au
15.2.5. aina nyingine ya hasara au uharibifu wa moja kwa moja au wa namna nyingine (ikiwa ni pamoja na, kwa mfano, hasara ambayo isingeweza kufikiriwa wakati wa kuanza uhusiano wetu).
15.3. Wajibu wa juu kabisa wa Bolt kwako kwa jumla kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa

hautazidi shilingi za kitanzania milioni moja (TZS. 1,000,000). Kiwango hiki kitatumika bila kujali idadi ya madai yaliyofanywa au idadi ya matukio yaliyosababisha wajibu huo.

15.4. Vikwazo vyote na misahama ya uwajibikaji viliyowekwa kwenye Masharti haya ya Jukwaa vitatumika kwa kiwango cha juu kabisa kinachoruhusiwa na sheria.

15.5. Hakuna chochote katika Masharti haya ya Jukwaa kinachozuia au kuondoa wajibu wa Bolt kwenye:

15.5.1. kifo au majeraha kwa mtu vilivyosababishwa na uzembe wa Bolt; au

15.5.2. wajibu mwingine wowote ambao hauwezi kuzuilika au kusamehewa kisheria.

**16. Vipengele vingine vya Muhimu**

Haki Miliki

16.1. Haki miliki zote, alama za biashara, haki za kubuni, na haki nyingine miliki katika Jukwaa la Bolt ikihusisha msimbo wa chanzo, hifadhidata, alama ya picha, miundo ya kuona (kwa pamoja, “Haki Miliki”) zinamilikiwa na, au zimepewa leseni kwa Bolt. Kwa kutumia Jukwaa la Bolt, haupewi haki yoyote ya umiliki kwenye haki miliki. Haupaswi kutumia, au kuruhusu matumizi ya Haki Miliki bila kibali cha Bolt kwa maandishi.

Notisi

16.2. Isipokuwa kama imeelezwa tofauti katika Masharti haya ya Jukwaa, notisi kwa Bolt kuhusiana na Masharti haya ya Jukwaa zitatolewa kwa njia ya maandishi kwenda Bolt kwa anuani iliyosajiliwa: Operesheni za Bolt, OÜ at Vana-Lõuna Tallinn 15, 10134, Estonia.

16.3. Bolt inaweza kutoa notisi kwako kuhusiana na Masharti haya ya Jukwaa kwa barua au barua pepe, kwa kutumia taarifa za mawasiliano za hivi karibuni ulizotoa kwetu kwa nyakati tofauti, au - kama wewe ni Dereva - kupitia Programu ya Dereva.

16.4. Isipokuwa kama imeelezwa tofauti katika Masharti haya ya Jukwaa, notisi zitakazotolewa kuhusiana na Masharti haya ya Jukwaa lazima zitolewe kwa Kiswahili au Kiingereza na na itachukuliwa kuwa zimewasilishwa ipasavyo:

16.4.1. kama imekabidhiwa kwa mkono, pale ambapo notisi itaachwa kwenye anuani inayohusika;

16.4.2. kama imetumwa kwa njia ya posta, siku inayofuata baada ya kuituma;

16.4.3. kama imetumwa kwa barua pepe, muda ambao barua pepe imetumwa; au

16.4.4. kama imetumwa kupitia Programu ya Dereva, muda ambapo notisi hiyo itakuwa kwako kupitia Programu ya Dereva.

16.5. Endapo muda ambao notisi inachukuliwa kuwasilishwa kwako ipasavyo kwa mujibu wa kipengele cha {16.4} itakuwa ni baada ya saa 11:00 jioni katika siku yoyote, au katika muda wowote kwa siku Jumamosi, Jumapili, au sikukuu, notisi hiyo itachukuliwa kuwa iliwasilishwa ipasavyo saa 03:00 asubuhi ya siku inayofuata ambayo siyo Jumamosi, Jumapili au sikukuu.

Utekelezaji

16.6. Bolt, kwa busara na kwa nia njema, inaweza inaweza kuamua kama kuna uvunjifu wa Masharti haya ya Jukwaa. Haki yoyote auhiari iliyotolewa au aliyonayo Bolt katika Masharti haya ya Jukwaa inaweza kutumiwa ipasavyo.

16.7. Bila kuzuia haki nyingine yoyote au uhiari uliotolewa kwa Bolt kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa, Bolt kwa busara na kwa nia njema, inaweza kuamua kama kitendo ni Kitendo cha Haramu cha Kidanganyifu Kilichokatazwa.

Migogoro

16.8. Katika mazingira ambayo Bolt:

16.8.1. imetoa maudhui kwenye Jukwaa la Bolt (tazama kipengele {4.2})

16.8.2. imesimamisha kuingia kwenye Jukwaa la Bolt (tazama kipengele cha {12})

16.8.3. imefungia kuingia kwenye Jukwaa la Bolt (tazama kipengele cha {13})

16.8.4. imechukua uamuzi mwingine kulingana na Masharti haya ya Jukwaa ambao hukubaliani nao;

Unaweza kuwasilisha lalamiko au ukaomba marejeo ya uamuzi uliojulishwa kwako kupitia Programu ya Dereva.

16.9. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa kisheria, migogoro yoyote inayotokana na au inayohusiana na Masharti haya ya Jukwaa ambayo haitatuliwa kupitia mfumo wa ndani wa kutatua migogoro, itawasilishwa kwenye mahakama za Tanzania, ambazo zitakuwa na mamlaka pekee.

Washirika Wetu

16.10. Unakubali kuwa Bolt inaweza kugawa, kuhamisha au kurejea haki zetu chini ya Masharti haya ya Jukwaa muda wowote pasipo kupata ruhusa yako, na kuwa tunaweza kutoa utekelezaji wa wajibu wetu au kuteua washirika wetu kutumia haki zetu chini ya Masharti haya ya Jukwaa. Hii haitaathiri haki zako au wajibu wetu chini ya Masharti haya ya Jukwaa.

Kodi ya Ongezeko la Thamani

16.11. Malipo yote, kiasi na kiwango kilichotolewa kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa zinajumuisha kodi ya ongezeko la thamani husika, isipokuwa kama imeelezwa tofauti.

Tafsiri

16.12. Vichwa vyote vya Habari na maneno yaliyoelezewa katika Masharti haya ya Jukwaa ni kwa ajili ya marejeleo tu na haiathiri tafsiri ya kifungu chohote.

16.13. Katika Masharti haya ya Jukwaa, isipokuwa ilipoelezwa tofauti:

16.13.1. rejeleo la "kipengele” inamaanisha kipengele ndani ya Masharti haya ya Jukwaa;

16.13.2. rejeleo kwa “mhusika” inamaanisha mhusika katika Masharti haya ya Jukwaa, na “wahusika” itatafsiriwa ipasavyo;

16.13.3. maneno yaliyo katika umoja yanajumuisha wingi wake na kinyume chake;

16.13.4. rejeleo kwa jinsia moja inahusisha jinsia zote;

16.13.5. rejeleo kwa “mtu” inalenga binadamu, kampuni, ushirika, asasi, au taasisi nyingine ya kisheria;

16.13.6. marejeleo kwa “ikiwemo” au maelezo kama hayo hayazuii vitu vingine kujumuishwa.

16.14. Endapo kifungu chochote katika Masharti haya ya Jukwaa kitakutwa au kuamuliwa na mahakama au chombo kingine chenye mamlaka kuwa hakiwezi kutekelezeka, wahusika wanakubali kukibadilisha kifungu hicho na kifungu kilicho sahihi na chenye kutekelezeka, kadri itakavyowezekana, kulinda lengo la awali na lenye maana kibiashara.

16.15. Endap kutakuwa na mgongano baina ya Masharti haya ya Jukwaa na makubaliano au mpango mwingine kati yako na Bolt, Masharti haya ya Jukwaa yatafuatwa labda kama imeelezwa tofauti.

16.16. Bolt inafanya kazi kama mtoaji wa Jukwaa mtandaoni kwa ajili ya huduma ya kuunganisha na machaguzi. Hivyo:

16.16.1. Hakuna chochote katika Masharti haya ya Jukwaa kinalenga kuonesha au kuamua kuwa Watoa Huduma au Madereva (Pamoja na Madereva Walioteuliwa) wanao wana wajibu kwa Bolt kufanya au kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni, au kwamba wanao uhusiano wa kiajira na Bolt.

16.16.2. Endapo kifungu chochote Masharti haya ya Jukwaa kitakutwa au kuamuriwa na mahakama au chombo kingine chenye mamlaka kuonesha wajibu binafsi wa kufanya au kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni au kuonesha uwepo wa mahusiano ya kiajira na Bolt, wahusika wanakubaliana kubadilisha kifungu hicho kwa kifungu kingine kilicho sahihi na kinachotekelezeka kitakachofuta mwelekeo huo, na kwa jinsi inavyowezekana, kutunza lengo la awali na lenye matokeo ya kibiashara.

Mamlaka

16.17. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, Masharti haya ya Jukwaa na matumizi yako ya Jukwaa la Bolt vitaongozwa, na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

**17. Farahasa ya maana ya maneno**

Katika Masharti haya ya Jukwaa, maana zifuatazo zitatumika:

17.1. 'Salio la Akaunti' inamaanisha jumla ya malipo yaliyokusanywa na Bolt kwa niaba yako, kutoa jumla ya kiasi kinacholipwa kwa Bolt, kama inavyokokotolewa kwa mujibu wa kipengele cha {9.1}.

17.2. 'Dereva Aliyeteuliwa' inamaanisha mtu aliyesajiliwa na kuteuliwa na Mtoa Huduma kama Dereva kwa mujibu wa kipengele cha {6}.

17.3. Bolt' ('sisi'/'yetu') inamaanisha Shughuli za Bolt OÜ iliyopo kwenye anuani iliyosajiliwa ya Vana-Lõuna Tallinn 15, 10134, Estonia.

17.4. 'Jukwaa la Bolt' inamaanisha teknolojia ya mfumo iliyotengenezwa na Bolt – ikiwemo Programu ya Dereva – ambalo kupitia humo Huduma za Usafiri Mtandaoni zinakutanishwa ndani ya Masharti haya ya Jukwaa, na kupitia vifaa vingine, taswira au huduma zinaweza kuwepo au kuunganishwa.

17.5. 'Ada ya Kughairisha' inaaanisha ada itakayotozwa na wewe kwa Wateja endapo Mteja ataahirisha ombi au kushindwa kwa namna nyingine kuingia kwenye mpango wa Huduma za Usafiri Mtandaoni baada ya Muda wa Kusubiri kuisha kama ilivyoelezwa katika vipengele {5.16} na {5.17}.

17.6. 'Makundi' inamaanisha makundi ya Huduma za Usafiri Mtandaoni yaliyopo kwenye Jukwaa la Bolt katika soko (inayoweza kuhusisha, kwa mfano, ikiwemo makundi ya 'magari ya umeme' au 'magari ya hadhi maalumu') na 'Kundi' inamaanisha aina yoyote katika hivyo.

17.7. 'Ada ya Usafi' inamaanisha ada inayotozwa na wewe kutoka kwa Wateja katika mazingira pale Msafiri amechafua gari wakati wa utoaji wa Huduma za Usafiri Mtandaoni kama ilivyoeelezwa zaidi katika vipengele {5.18} na {5.19}.

17.8. 'Kipindi cha Kukusanya' inamaanisha kipindi ambacho:

17.8.1. kinaanza pale Dereva anaonesha (kupitia Programu ya Dereva) tayari wake wa kutoa au kutimiza Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa Mteja husika kadri ya ombi la Mteja la Huduma za Usafiri Mtandaoni; na

17.8.2. inakoma muda wa kuanza kwa Kipindi cha Safari au, kama ni mapema, pale ombi la Huduma za Usafiri Mtandaoni limeghairishwa au limesitishwa.

17.9. 'Kamisheni' inamaanisha kamisheni inayolipwa na wewe kwa Bolt kwa kupata huduma za Bolt zilizotolewa na wewe kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa kama ilivyoelezwa kwenye kipengele {8}.

17.10. 'Bidhaa Zisizo na Kamisheni' inamaanisha ada na malipo ambayo Kamisheni haitozwi ambazo ni takrima zote, Ada ya Usafi na Malipo ya Tozo.

17.11. 'Kipindi cha Kusubiria' inamaanisha (kama inavyotumika) kipindi kilichowekwa katika Jukwaa la Bolt kuanzia pale Dereva anapoonesha (kupitia Programu ya Dereva) utayari wake wa kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa Mteja husika kufuatana na ombi la Mteja la Huduma za Usafiri Mtandaoni.

17.12. 'Mteja' inamaanisha mhusika anayeomba (na anaweza kupewa) Huduma za Usafiri Mtandaoni.

17.13. 'Huduma za Usafirishaji' inamaanisha huduma za usafirishaji zinazotolewa na Watoa Huduma kwa Wateja kwa ajili ya kusafirisha bidhaa kutoka eneo la kupokelea kwenda eneo la mwisho/kikomo bila kusafirisha Msafiri, kama ilivyoelezwa katika vipengele {5.28} na {5.32}.

17.14. 'Tabia ya Kibaguzi' inamaanisha tendo lolote – ikiwemo kauli, matendo, na vitendo kwa wengine – ambacho kinaonesha upendeleo, iathari, au chuki na sifa zinazolindwa kama rangi,

ukabila, uraia, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia, dini, ulemavu au umri.
17.15. ‘Dereva’ inaamisha mtu aliyesajiliwa na Bolt na wewe kufikia na kupitia fursa za kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa niaba yako ikiwemo (kama inavyotumika):
17.15.1. wewe; na/au
17.15.2. Madereva Walioteliuwa;
17.16. ‘Programu ya Dereva’ inamaanisha programu ya simu ya mkononi inayotolewa na Bolt ili kupitia fursa za utoaji wa Huduma za Usafiri Mtandaoni.
17.17. ‘Malipo ya Awali’ inamaanisha malipo ya mapato yako kabla ya muda stahiki wa malipo kama ilivyoeelezwa zaidi kwenye vipengele vya {9.5} hadi {9.7} kwa pamoja.
17.18. ‘Nauli’ inamaanisha gharama inayolipwa kwa ajili ya Huduma za Usafiri Mtandaoni.
17.19. ‘Kipindi cha Safari’ inamaanisha kipindi kitumikacho:
17.19.1. kuanzia Dereva anapomchukua abiria au bidhaa, kama inavyotumika, kutoka eneo la kupokelea kwa ajili kusfirisha hadi eneo la mwisho/kikomo lililoombwa; na
17.19.2. inakoma pale Huduma za Usafiri Mtandaoni inaisha au kufikia mwisho kwa sababu nyingine yoyote.
17.20. ‘Abiria’ inamaanisha mtu yeyote ambaye anasafirishwa au atakaye safirishwa kama abiria kwa mujibu wa kifungu cha Huduma za Usafiri Mtandaoni.
17.21. ‘Njia ya Malipo’ inamaanisha njia ya malipo ya kuhamisha kiasi kinacolipwa kwako kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa, taarifa ambazo umezitoa kwa Bolt.
17.22. ‘Masharti ya Jukwaa’ inamaanisha ujumla wa vigezo na masharti haya yanayojulikana kama ‘Masharti ya Jukwaa kwa ajili ya Huduma za Usafiri Mtandaoni: Watoa Huduma (Tanzania)’.
17.23. ‘Matendo ya Udanganyifu Yaliyokatazwa’ inamaanisha matumizi yoyote ya Jukwaa la Bolt yanayoonesha nia – au jaribio lolote – la kudanganya, kuharibu, kuumiza mtu yeyote au Jukwaa la Bolt wenyewe, au kuharibu au kutoa sifa yoyote ya nyongeza kinyume cha utaratibu kwenye Jukwaa la Bolt. Hii inahusisha:
17.23.1. ombi, kubalio au kumaliza Huduma za Usafiri Mtandaoni katika namna ambayo inaonesha kuwa iliyopitiliza, ya kutengeneza au iliyopangwa visivyo; na
17.23.2. tabia inayojirudia inayoonesha kuwa imetengenezwa kudanganya uhalisia wa uhitaji au nia ya kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni.
17.24. ‘Vipindi vya Kuomba Huduma’ inamaanisha kwa pamoja (kuhusiana na ombi la Huduma za Usafiri Mtandaoni) Kipindi cha Kukusanya, na endapo Huduma za Usafiri Mtandaoni imeanza, Kipindi cha Safari.
17.25. ‘Mtoa Huduma’ inamaanisha mtu au taasisi ambayo imejisajili kwa Bolt ili kufikia na kupitia fursa za kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni ndani ya Tanzania kwa faida yao wenyewe.
17.26. ‘Huduma za Usafiri Mtandaoni’ inamaanisha huduma za usafirishaji zinazotolewa na Watoa Huduma kwa Wateja ambazo zinapangwa kupitia Jukwaa la Bolt (ikiwemo Huduma za Usafirishaji).
17.27. ‘Malipo ya Tozo’ inamaanisha malipo yanayopaswa kulipwa kwa Watoa Huduma kama tozo ya ziada kwa sababu ya njia ya Huduma za Usafiri Mtandaoni inayosababisha gharama ya ziada au usumbufu kwa mfano safari kupitia barabara na madaraja ya kulipia au safari zinazohitaji ada ya kuegesha gari kwenye kiwanja cha ndege.
17.28. ‘Watumiaji’ inamaanisha watumiaji wote na wanufaika wa Jukwaa la Bolt ikiwemo Watoa Huduma, Madereva, Wateja na Abiria.
17.29. ‘Wewe’ inamaanisha Mtoa Huduma anayehusika na Masharti haya ya Jukwaa.

Mwisho wa Masharti ya Jukwaa